© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

DIBAJI:
Anwani hii ya "Mama Zao Waumini", makusudio yake ni wake zake Mtume (S.A.W). Mwenyezi Mungu (S.W) ndie aliewapa wao anwani hiyo: **"Nabii ana haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao, na wakeze ni mama zao."**

Mama za waumini wanastahiki heshima na staha mahsusi. Wao ndio wanawake ambao Mwenyezi Mungu aliowachagua kuwa ni wasiri wa jamii ya Mtume (S.A.W). Napia wao ndio waliotupasha kuhusu sehemu kubwa ya elimu kutoka kwa mume wao, Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W). Kama ilivyo baina ya mtu na mamake, Mwenyezi Mungu (S.W) ametuharimishia kuwaowa yeyote miongoni mwao (Mama za Waumini) baada ya kuondoka Mtume (S.A.W): **"Wala haikupasieni (haitakikani) kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala kuwaowa wake zake baada yake kabisa. Hakika jambo hilo ni (dhambi) kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu."** Katika sura hii, tutagusia kuhusu hali za kila mmoja wa Mama zao Waumini kwa muhtasari tu. Na sababu ya hayo ni uhusiano wao muhimu katika kutusimulia mengi ya tuyajuayo kuhusu maisha ya ndoa ya Mtume (S.A.W). Kumbukumbu zetu kuhusiana na hayo ni:

- Siyar A`lam in-Nubal`a (Habari za maisha ya watu bora), al-Hafidh Shams ud-Din adh-Dhahabi, Mu'assasat ur-Risalah, Beirut, 1419 (1998).
- Tarajimu A`lam in-Nisaa (Habari za maisha ya wanawake mashuhuri), Radhwaan Da'bul, Mu'assasat ur-Risaalah, Beirut, 1419 (1998)
- At-Taarikh ul-Islami (Tarekh ya Uislamu), Mahmud Shakir. Al-Maktab ul-Islami, Berut, 1411(1991).

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Khadijah Bint Khuwaylid:

Bibi Khadijah Bint Khuwaylid (R.A) alikuwa ni mwanamke bora kuliko wanawake wote wa wakati wake. Alikuwa ni binti ya Khuwaylid Bin Asad Bin Abd il-'Uzza Bin Qusayy Bin Kilab kutokamana na Quraysh. Kabla ya Uislamu, alikuwa akiitwa at-Taahira (alie Tahirika). Khadijah alikuwa ni mwanamke tajiri, hivyo basi, akamuajiri Mtume (S.A.W) kuisimamia biashara yake ya msafara kuelekea Sham. Baada ya kushuhudia uaminifu wake na usimamizi mzuri, Bibi Khadijah alijitolea nafsi yake ili aolewe na Mtume (S.A.W), nae akaungama.

Kabla ya kuolewa na Mtume (S.A.W), aliolewa na Abu Halah Bin Zurarah at-Tamimi, kisha akaolewa na 'Atiq Bin 'Abid Bin 'Abdillah Bin 'Umar Bin Makhzum. Mtume (S.A.W) alipomuowa Bibi Khadijah, alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano nae Bibi Khadijah alikuwa na miaka arubaini.
Alimzalia Mtume (S.A.W) watoto saba; waume watatu (Al-Qasim, At-Tayyib, na At-Tahir) na wanawake wanne (Ruqayyah,Zaynab,Umm Kulthum na Faatimah). Ingawaje hawa watoto wa kike ni wenye kujulikana na ni kitu kilichothibitishwa, watu wa tarekh wamehitalifiana kuhusu watoto wa kiume-mpaka baadhi yao wakasema yakwamba hakupata mtoto wa kiume kabisa kutoka kwa Bibi Khadijah, na wengine wakasema alimzalia Qasim (na kadhalika). Watoto wa kiume walifariki mapema katika hali ya utoto na watoto watatu wakwanza wa kike walifariki wakiwa al-Madina wakati wa uhai wa Mtume (S.A.W). Faatimah (R.A.) alifariki miezi michache baada ya babake.

Bibi Khadijah ndie mtu wa kwanza kabisa kumuamini Mtume (S.A.W) na kumsaidia. Mara kwa mara Jibril (A.S.) alikuwa akimuuliza Mtume (S.A.W) amsalimie Bibi Khadijah: **"Ewe Khadijah, Jibril akusalimu." "Ewe Muhammad, mwambie Khadijah asalimiwa na Mwenyezi Mungu."** Khadijah ni mmoja kati ya wanawake watatu walotajwa na Mtume (S.A.W) kuwa wamekamilika: **"Walokamilika miongoni mwa wanaume ni wengi (kwa Imani, Tabia na Taqwa), lakini wanawake (watatu tu) ndio walokamilika: Asiyah mkewe Fir'auni, Maryam Bint 'Imran, na Khadijah Bint Khuwaylid. Na ubora wa ''Aaisha juu ya wanawake wengine ni kama ubora wa tharid juu ya aina nyengine ya chakula."**

Vile vile Mtume (S.A.W) alimtaja yeye kama mmoja wa wanawake wanne bora katika nyakati zote: **"Bora wa wanawake katika ulimwengu mzima ni wanne: Maryam Bint 'Imran, Khadijah Bint Khuwaylid, Faatimah Bint Muhammad (S.A.W) na Asiyah mkewe Fir'auni."** Mtume (S.A.W) hakuwahi kuowa mwanamke mwengine kabla ya Khadijah na wala hakuongeza mke mwengine wakati alipokuwa nae. Alipokufa alikuwa na majonzi makubwa.

'Aaisha (R.A.) akasema yakwamba alipokuwa Mtume (S.A.W) akimtaja Khadijah, jambo hilo lilikuwa halimchoshi na akimsifu na kumuombea msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu . Siku moja wivu wake ulimzidi akasema, "Mwenyezi Mungu amekupa alie bora kuliko huyo mwanamke mzee." Aaisha aliziona alama za kughadhibika juu ya uso wa Mtume (S.A.W). Akahisi kuwa amekosea kutamka

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

hivyo, basi akajiambiya nafsi yake,"Ewe Mola wangu, sitosema tena chochote kibaya kumuhusu Khadijah." Mtume (S.A.W) alipofahamu kuhusu majuto ya 'Aaisha akasema: **"Vipi utasema hivyo! Wallahi, yeye ameniamini mimi wakati watu waliponikataa, na akanihifadhi mimi wakati watu waliponifukuza. Na nimebarikiwa na watoto kutokamana na yeye, ambapo nyinyi (wake wengineo) mumenyimwa kupata watoto kutokamana na mimi."** Akaongezea Aisha, "Aliendelea kuyakariri maneno hayo, usiku na mchana, kiasi cha mwezi mzima." Kwenye riwaya nyengine, 'Aaisha (R.A) akasema kuwa Mtume (S.A.W) amesema: **"Laa! Mwenyezi Mungu hakunipa alie bora badala yake. Aliniamini mimi wakati watu waliponikanusha,akanifanya kuwa mshirika kwenye mali yake wakati watu walipokataa kunipa na Mwenyezi Mungu akaniruzuku na watoto kutokamana na yeye ambapo Akanikatalia watoto kutokamana na yeyote mwengine.**

Bibi Khadijah ana daraja bora miongoni mwa wanawake waislamu wa nyakati zote. Hiyo ni kwa sababu hakuwa na msimamo wa kusitasita alipokuwa akimsaidia mbora wa waume alowahi kuwa nao. Alimuamini , akajitolea kwa hali na mali juu yake; na akampa moyo kwenye wakati wa mashaka. Mwenyezi Mungu alimjaaliya Jannah kwa msimamo alokuwa nao kwenye maisha ya Mtume (S.A.W), na kwa sababu hiyo katika maisha ya kila muislamu. Mtume (S.A.W) alikuwa akiuenzi ukumbusho wake na kuudumisha uhusiano na marafiki zake baada ya kufa kwake. Mwenyezi Mungu akamjaalia kupata nafasi yakuwa mama wa watoto wote wa Mtume (S.A.W). Wanawake wote waislamu wanatakikaniwa wafaidike kutokamana na mfano wa Bibi Khadijah.

Bibi Khadijah (R.A.) alikufa miaka mitatu kabla ya Hijrah, na akazikwa mahala paitwapo Al-Hajun (mlima juu ya Makkah). Nae akifa alikuwa na umri wa miaka sitini na tano.

Saudah Bint Zam'ah:

Saudah Bint Zam'ah Bin Qays (R.A.) alikuwa ni wa kabila la Quraysh. Alikuwa awali ameolewa na As-Sakraan Bin 'Amr al-'Amiri nao wote walikuwa ni miongoni mwa watu walosilimu mwanzoni mwa Uislamu. Alihajiri na mumewe kuelekea Habasha (Abyssinia). Baada ya kurudi kwao, mumewe akafa na Mtume (S.A.W) akamuowa. Alimuowa Makkah wakati wa Ramadhan katika mwaka wa kumi wa Utume wake. Saudah (R.A.) alikuwa kwenye takriban umri wa hamsini alipo-olewa na Mtume (S.A.W). Bila kukawiya baada ya Hijrah, Mtume (S.A.W) alimchukuwa kuja kuishi nae huko al-Madina.

Saudah (R.A.) alikuwa ni mwanamke wakwanza kuolewa na Mtume (S.A.W) baada ya Bibi Khadijah (R.A.). Alikuwa ni mkewe pekee kwa muda wa miaka mitatu-mpaka alipomuowa 'A'Aaisha (R.A.). Kwa ajili ya umri wake mkubwa, Saudah (R.A.) akaishiwa na matamanio juu ya wanaume na akajihisi yakwamba hatoweza tena kumridhisha kikamilifu Mtume (S.A.W). Kwahivyo, Mtume (S.A.W) alipomuowa 'Aaisha (R.A.), Saudah akajitolea siku zake na Mtume (S.A.W) kwa 'Aaisha ili

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

kumridhisha-iwapo alikuwa na fikira zozote za kumtaliki.

Saudah (R.A.) alikuwa ni mwanamke mahashumu, mkubwa na mwenye tabia nzuri. Alikufia al-Madina kufikia mwishoni mwa khilafa ya 'Umar (R.A).

Kuolewa kwa 'Aaisha (R.A.)

'Aaisha(R.A.) alikuwa ni binti wa as-Siddiq (mkweli wa wakweli), Abu Bakr 'Abdullah (R.A.) Bin Abi Quhafah 'Uthman Bin 'Amir Bin K'ab Bin Sa'ad Bin Taym Bin Murrah kutoka kwenye kabila la Quraysh. Nae ni mwanamke alie na kiwango kikubwa zaidi cha elimu katika Ummah mzima pasi na pingamizi yoyote. Mamake alikuwa ni Umm Ruman Bint 'Amr Bin 'Uwaymir kutoka katika kabila la Kinaana.

'Aaisha (R.A.) alizaliwa katika Uislamu. Alisema, "Sikuwahi kuwaona wazazi wangu isipokuwa walikuwa wakifuata Dini (Uislamu). Alikuwa ni mdogo wa Faatimah (R.A.) kwa miaka minane. Ndoa yake ilitekelezwa baina ya Mtume (S.A.W) na Babake kwa muda wa miaka miwili kabla ya Hijrah. Na huo ndiwo mwaka ambao Mtume (S.A.W) alimuowa Saudah (R.A.). Alisafiri na wazazi wake kuelekea al-Madina, na Mtume (S.A.W) akaitimiliza ndoa (akamuingilia) upesi baada ya vita vya Badr, katika mwezi wa Shawwal. Hapo alikuwa na umri wa miaka tisa. Akaishi na Mtume (S.A.W) kwa muda wa miaka tisa. Ikapokewa kutoka kwa Aisha (R.A.): "Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) aliniowa mimi (kufunga ndoa tu) muda mfupi baada ya kufa Khadijah,nilipokuwa na umri wa miaka sita. Nikaletwa kuonana nae (kuitimiza ndoa) nlipofika miaka tisa. Baadhi ya wanawake wakanijia nilipokuwa nacheza kwenye bembeya na nywele zangu ndefu mpaka mabegani. Wakanitayarisha na kunipamba, kisha wakanipeleka kwake."

Asmaa' Bint Yazid Bin As-Sakran akaeleza yakwamba alimpambia Mtume (S.A.W) 'Aaisha, kisha akamkaribisha aje amuone. Akaja na akaketi karibu yake. Mtume (S.A.W) akapewa kikombe kikubwa ya maziwa. Akanywa kiasi na mengine akampa nae 'Aaisha anywe. 'Aaisha akaangusha kichwa chake kwa haya nyingi sana mpaka Asmaa' akamkaripia akasema: "Usimkatalie Mtume wa Mwenyezi Mungu akupacho! Hapo basi akachukuwa kikombe na akanywa kidogo. Kisha Mtume (S.A.W) akamwambia, **"Wape nao rafiki zako."** Asmaa' akasema, " Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwanza kichukuwe wewe hicho kikombe na unywe kutoka humo, kisha unipe mimi kwa mikono yako." Mtume (S.A.W) akakichukua hicho kikombe, akanywa na kisha akampa. Asmaa'. Akaketi chini, akakituliza kikombe juu ya magoti yake na akaanza kukizungusha mpaka akaeka mdomo wake kwenye ukingo wa kikombe pale-pale alipokunywia Mtume (S.A.W) Kisha Mtume (S.A.W) akawaelekea wanawake alokuwa nao na akasema **"Wape nao marafiki zako."** Wakasema wale wanawake, "Sisi hatuna haja nayo." Mtume (S.A.W) akawajibu: **"Musichanganye njaa na uwongo."**

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

UJANA WAKE 'AAISHA (R.A.)

Mtume (S.A.W) aliuona utoto alokuwa nao 'Aaisha katika hali yake ya kimaumbile kwenye miaka yake aloishi nae hapo mwanzoni, akamchukulia kwa kadiri ya fahamu zake. Akatuhadithia 'Aaisha: "Nilikuwa nikipenda kuchezea madoli (watoto wa bandia) na baadhi ya marafiki zangu wasichana wadogo, walikuwa wakija na kucheza na mimi. Alipokuwa Mtume (S.A.W) akija nyumbani, walikuwa wakijificha; na anapotoka wao hurudi. Na Mtume (S.A.W) ndie alokuwa akiwaleta kuja kucheza na mimi."

Pia ikapokewa kutoka kwa 'Aaisha (R.A) kuwa aliporudi Mtume (S.A.W) kutoka kwenye vita vya Tabuk (au Khaybar), alikuwa na shubaka (mahali pa kupumzikia penye uvuli) ilofinikwa na pazia. Upepo ukaipeperusha ile pazia kidogo na hapo ndipo walipodhihirika Madoli (watoto wa bandia). Akauliza Mtume (S.A.W), **"Ni nini hino ewe 'Aaisha?"**. Nae akajibu, "Haya ni madoli yangu". Akaona baina yao, kuna farasi mwenye mbawa za ngozi na akauliza, **"Ni kitu gani hichi ambacho ninachokiona baina yao?"** Akajibu 'Aaisha, "Ni farasi." Mtume (S.A.W) akauliza**"na ni kitu gani hicho juu yake?"** Akajibu, "Ni mbawa mbili." Akamaka Mtume (S.A.W), **"Farasi na mbawa mbili?"** Akasema 'Aaisha, " Hujawahi kusikia wewe kuwa Suleiman alikuwa na Farasi wenye mbawa?". Mtume (S.A.W) akacheka mpaka 'Aaisha (R.A) akayaona magego yake.

Akahadithia 'Aaisha (R.A.) kwamba, siku moja alipokuwa kwenye umri wa ujana aliwahi kusafiri na Mtume (S.A.W). Walipofika mahali fulani, aliwaamuru maswahaba zake watangulie mbele, akawaambia, **"Hebu tangulieni nyinyi."** Kisha akamwambia 'Aaisha, **"Haya hebu njoo tushindane."** Wakakimbizana na 'Aaisha na 'Aaisha akaebuka mshindi. Miaka michache baadae, alipopata mwili 'Aaisha, wakawahi kusafiri tena kama ile mara ya kwanza. Mtume (S.A.W) akawaambia maswahaba zake, **"Hebu tangulieni nyinyi**. Kisha akamwambia 'Aaisha, **"Haya, njoo tushindane."** Wakakimbizana, na Mtume (S.A.W) akashinda. Akasema kumwambia 'Aaisha, **"Huu ni ushindi wa kulipiza (mashindano) ya mwanzo."** 'Aaisha (R.A.) alinukuu siku moja kuwa ujumbe wa Mahabashi walikuja kwa Mtume (S.A.W). Ilipokuwa siku ya 'Idd, walicheza ndani ya msikiti na mikuki yao. 'Umar (R.A.) akaazimia kutaka kuwakataza, lakini Mtume (S.A.W) akamwambia, **"Wawache waendelee."** Mtume (S.A.W) alisimama kwenye mlango wa chumba cha 'Aaisha uelekeao ndani ya msikiti na akamwita 'Aaisha aje asimame nyuma yake ili atizame mchezo wao. Akaongezea 'Aaisha: "Walicheza ndani ya msikiti. Mtume (S.A.W) alitumia vazi lake la juu kunitanda nalo huku nikitizama. Nilisimama nyuma yake; nikaegeza kidevu changu juu ya mabega yake na uso wangu umeegemea uso wake. Alikuwa ni mstahamilivu mno katika kusubiri kwake mpaka nikakinai nikataka kuondoka mimi mwenyewe-kwahivyo inatakikana muelewe matakwa ya msichana mdogo (ya machezo)."

BIKIRA WA KIPEKEE (MWANAMWALI)

'Aaisha (R.A.) alikulia kuwa mwanamke mzuri alie na sifa njema. Hiyo ndio sababu akaitwa Al-Humayra, Cheupe.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Mtume (S.A.W) hakuoa mke bikra isipokuwa 'Aaisha (R.A.) peke yake; na alikuwa 'Aaisha akijivunia kwalo. Wakati mmoja alimuuliza , "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, endapo ulikuwa uchukue kituo cha mapumziko. Kwenye bonde ukaona miti malishoni iliyoparuzwa na wanyama na mti mmoja ukauona haujawahi kukurubiwa, Jee, utamlisha wapi ngamia wako?. Akajibu, **"Kwenye mti ambao haujaparuzwa (haujaliwa)"**. 'Aaisha akasema, " Basi mimi ndie huo mti."

MKE ALOPENDWA ZAIDI

Mtume (S.A.W) alimpenda zaidi 'Aaisha (R.A.) kuliko wake zake wote. 'Amr Bin al-'As (R.A.) akatuhadithia yakwamba alimuuliza Mtume (S.A.W), "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni nani miongoni mwa watu apendekezae zaidi kwako?". Akajibu:**"'Aaisha"**. Akauliza tena, "Jee, miongoni mwa wanaume?" Akajibu,**"Babake 'Aaisha"**. Mapenzi ya Mtume (S.A.W) kwa 'Aaisha yalikuwa ni dhahiri, yakijulikana waziwazi miongoni mwa waislamu- na alikuwa (S.A.W) hapendi isipokuwa kilicho kizuri. Kwahivyo akachagua watu wawili bora katika umma huu kama vipenzi vyake. Mtu yeyote atakaewapenda hao, jambo hilo litaashiria mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake (S.A.W); na atakapowachukia (hao watu wawili), basi huyo hatostahiki mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume (S.A.W).

UBORA WAKE JUU YA WANAWAKE WENGINE

'Aaisha (R.A.) aliwashinda wanawake wengine kutokana na sifa zilizomfanya Mtume (S.A.W) mpaka akasema: **Ubora wa 'Aaisha juu ya wanawake wengine ni kama ubora wa tharid juu ya aina nyengine ya chakula."** Asili ya ubora huu imetokana na wahyi ambao ulomfanya Mtume (S.A.W) ampende yeye zaidi ya wake zake wote wengine.

Kama tutakavyo ona katika Sura ijayo, 'Aaisha (R.A.) ndie wa pekee miongoni mwa mama za waumini ambae Jibril (A.S.) alikuja na ujumbe (wahyi) kwa Mtume (S.A.W) hali ya kuwa amejifunika na tandiko moja pamoja nae ('Aaisha). Mara kwa mara, Mtume (S.A.W) alikuwa akimwambia: **"Ewe 'Aaisha, Jibril yuko hapa, na yuwakusalimia."**

MASINGIZIO MAKUBWA

Baada ya kuitambua daraja kubwa ya 'Aaisha (R.A.) kwenye moyo wa Mtume (S.A.W), wanafiki walijaribu kumvunjia heshima yake kupitia kwake ('Aaisha). Katika mwaka wa 5 baada ya Hijrah, Mtume (S.A.W) alipokuwa akirudi al-Madina kutoka kwenye vita vya al-Muraysi. 'Aaisha (R.A.) alikuwa nae, na alikuwa na umri wa miaka kumi na mbili. Kufikia karibu na safari hiyo, Jeshi lilisimama kwa mapumziko.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Muda mchache kabla ya kuondoka mahali hapo wakati wa usiku, 'Aaisha alijikuta ameupoteza mkufu wake, hivyo basi akaendoka mahali hapo ili kuutafuta kila mahali. Aliporudi, alikuta tayari msafara ushaondoka. Alijitanda nguo zake na akakaa kuwasubiri watu watakaorudi kumtafuta yeye. Baada ya muda, usingizi ulimchukua akalala.

Safwan Bin Al-Mu'attal (R.A.) alikuwa juu ya kipando chake nyuma ya kikosi cha jeshi akijitahidi kuwafikia. Alifika mahali alipokuwa 'Aaisha wakati wa asubuhi akamkuta pale amejikunyata na akamtambua mara moja. Akashuka kwenye kipando chake (ngamia) ili ampishe 'Aaisha apande; kisha yeye akaanza kutembea kwa miguu, akiwa mbele kumuongoza yule ngamia hatimae alikifikia kikosi kilipokuwa kimesimama pahali kwa mapumziko wakati wa mchana. Hii ilikuwa ni nafasi ya kufaa sana kwa kiongozi wa wanafiki, 'Abdullah Bin Abi Salul, na wafuasi wake kumsingizia 'Aaisha (R.A.), Mumewe (S.A.W) na Umma mzima kwa kumsuta eti amezini na Safwan.

Jambo hili lilimhuzunisha sana Mtume (S.A.W) na waislamu kwa mwezi mzima mpaka Mwenyezi Mungu akateremsha Aya kumi kuubainisha ukosefu wake wa hatia na kuwalaumu wote wale waloshiriki katika masingizio yake. Kisha Mtume (S.A.W) akamwambia 'Aaisha: **"Ama kwa kweli, Wallahi, Mwenyezi Mungu amekubainishia yakwamba huna hatia!"**

WIVU WA 'AAISHA

Licha ya mapenzi ya hali ya juu ambayo Mtume (S.A.W) alomuonyesha 'Aaisha (R.A.), 'Aaisha nae alikuwa na wivu mno juu ya Mtume (S.A.W) Matukio kadha yanayo onyesha hali hii yamenukuliwa katika Sura ifuatayo. Inashangaza kuona kama tulivyotaja mbeleni,kuwa wivu wake ulifika mpaka kwa khadijah(R.A.)aliekufa miaka mitatu kabla ya kuolewa kwake. Akasema: Sijawahi kuwa na wivu kwa mwanamke yeyote zaidi ya nilivyokuwa na wivu na Khadijah (R.A)- kutokana na alivyokuwa akitajwa mara kwa mara na Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W).

Ikapokewa kutoka kwa Anas na Umm Salamah (R.A.) kuwa wakati fulani alipokuwa Mtume (S.A.W) na baadhi ya maswahaba zake kwenye nyumba ya 'Aaisha (R.A.), Umm Salamah alipeana sahani ya chakula apelekewe Mtume (S.A.W). 'Aaisha (R.A.) alipokiona chakula hicho, aliokota jiwe la kiasi cha mkono wake, akaligonga na ile sahani na kuivunja sehemu mbili. Mtume (S.A.W) akaokota vigae vya ile sahani na akawaambia maswahaba zake:

"Kuleni-Mama-enu amefanya wivu! Kuleni Mama-enu amefanya wivu." Basi maswahaba zake wakala hicho chakula. Mtume (S.A.W) akaviweka vile vigae kwenye nyumba ya 'Aaisha, kisha akachukua sahani nzima ya 'Aaisha na kumpelekea Umm Salamah na akasema: **"Sahani inayolingana na sahani (iliovunjwa) na chakula kinacholingana na chakula (kilichomwagika)."**

'Aaisha (R.A.) akasimulia kuwa katika usiku mmoja, ghafula alijiona peke yake kitandani na Mtume wa Mwenyezi Mungu hayupo. Mara akamuona (yuwaswali),basi

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

hapo 'Aaisha (R.A.)akavipenyeza vidole vyake kwenye nywele za Mtume (S.A.W)(kuona iwapo ametoka kuoga). Akasema Mtume: **"Amma kwa hakika shetani wako amekujilia!".** 'Aaisha akauliza, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Jee, wewe unae shetani?". Akajibu: **"Na'am, ninae.lakini Mwenyezi Mungu alinisaidia mimi dhidi yake akasilimu."** Ikapokewa kutoka kwa 'Aaisha(R.A)kuwa ilitokea katika usiku mmoja alimkosa Mtume(S.A.W)na akadhania yakwamba amekwenda kwa mmoja wa wakeze. Akaanza kumtafuta na akamuona anaswali, akiwa kwenye ema kwenye *ruku'* au sujuud, akinong'ona:
"Subhaanaka wa-bihamdika, laa ilaha illa-anta-(kutakasika ni kwako, na shukrani ni kwako; Hapana Mola (apasae kuabudiwa kwa haki) isipokuwa Wewe."

Kisha 'Aaisha akasema, "Babangu na Mamangu na Wawe ni kikombozi chako: kwa hakika wewe uko kwenye hali moja (ya Ibadah) na mimi niko kwenye hali tofauti(ya wivu).

Akatuhadithia 'Aaisha (R.A.) yakwamba ilitokea katika usiku mmoja ambao ilikuwa ni zamu ya Mtume (S.A.W) kuwa katika nyumba yake. Mtume (S.A.W) akapanda kitanda kulala, akavua vazi lake la juu akavua viatu vyake na kuvieka karibu na miguu yake, kisha akaikunjua izar yake (vazi lake la chini) akajionyosha. Alisubiri kwa muda mpaka akadhani kuwa 'Aaisha tayari ameshapata usingizi, kisha akanyapa kwa utaratibu na kuchukuwa vazi lake la juu, akavaa viatu akafungua mlango na kutoka nje hatimae akaufunga mlango. 'Aaisha nae akavaa nguo zake haraka haraka, akavaa vazi lake la kichwa na kujitanda izar yake na kutoka mbio kumfuata Mtume(S.A.W).

Mtume(S.A.W) akaelekea Al-Baqi` , na alipofika akasimama kwa muda mrefu, kisha akainua mikono yake mara tatu. Baada ya kufanya hivyo, akageuka na 'Aaisha(R.A.) nae akageuka; akakaza mwendo na 'Aaisha nae akakaza mwendo; akaanza kukimbia na 'Aaisha nae pia akaanza mbio-mpaka wote wakawasili nyumbani pamoja. Kwa vile 'Aaisha (R.A) alikuwa mbele, aliingia mwanzo. Pindi alipojibwaga kitandani, Mtume (S.A.W) akaingia na akamaka, **"Una nini ewe 'Aaisha, mbona unahema na tumbo lako linapanda na kushuka (kwa pumzi)?"** Akajibu 'Aaisha(R.A) "Sikitu Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu". Mtume (S.A.W) akasema, **"Ema uniambie, au Mwerevu wa waerevu na Mjuzi wa wajuzi atanipasha habari."** Kwahivyo akasema, "Babangu na Mamangu na wawe ni kikombozi chako, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu," na kisha akamuelezea yalotokea. Mtume (S.A.W) akamuuliza. **"Kwa hivyo wewe ndie kile kitu cheusi kilichokuwa mbele yangu?"** 'Aaisha (R.A) akajibu, "Naam!" Mtume (S.A.W) akambonyeza kwa mzaha kwenye kifua chake, kisha akamwambia, **"Wewe ulikuwa ukidhania yakwamba, Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawatokufanyia usawa (kwa kupeana haki yako ya wakati kwa mke mwengine)?"** 'Aaisha (R.A.) akasema, "Mwenyezi Mungu anajua jambo lolote lenye kufichwa na watu. Mtume (S.A.W) akasema: **"Naam! Kwa hakika, Jibril alinijia mimi ulipoyaona mambo hayo. Akaniita kwa siri pasi na wewe kujua, nami nikaitikia mwito wake bila ya kukujulisha. Haikumpasa yeye kuingia nyumbani kwako baada ya wewe kuzivua nguo zako. Nilidhania labda ulikuwa umelala nikachukia kukuamsha, kwa kuhofia pengine utahisi**

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

upweke (kama ungelijua kuwa nilikuwa niondoke), Jibril aliniambia, "Mola wako yuwakuamrisha uwende kwa watu (waliokufa) huko al-Baqi` ili uwaombee msamaha."

'Aaisha(R.A.) akamuuliza Mtume(S.A.W), "Nisemeje katika maombi yangu kwao, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?". Mtume (S.A.W) akamfundisha aseme: **"As-Salamu 'alaa ahl id-diyari min al-Mu'minina wal-muslimin, wa-yarham Ullah ul-mustaqdimina minnaa wal-musta'akhirin, wa-inna insha 'Allah bikum laahiqun.**
Amani iwe juu ya wakaazi wa sehemu hizi miongoni mwa waumini na waislamu. Mwenyezi Mungu awarehemu, waliotangulia na watakao wafuata miongoni mwetu. Na kwa hakika tutakuwa pamoja nanyi apendapo Mwenyezi Mungu."

VITA VYA AL-JAMAL (NGAMIA)

Katika tarehe 18 wa mwezi wa Dhul-Hijjah, mwaka wa 35 H, 'Uthmaan (R.A) aliuwawa kutokana na hila za 'Abdullah Bin Saba' na maadui wengine wa Uislamu. Siku chache baadae, Ali (R.A) alichaguliwa kuwa Khalifa mpya. Ali, 'Aaisha na baadhi ya Maswahaba wengine wakubwa, wakakusudia kusuluhisha matatizo kufuatia mauwaji ya 'Uthman (R.A) -muhimu zaidi, kuwatafuta wauwaji na kuustawisha (kuurudisha) tena ukhalifa.

Kwa hali yoyote ile, Ibn Saba' na wafuasi wake waliendelea na njama zao, hatimae wakafaulu kuwafitini maswahaba na kuanza kupigana wenyewe kwa wenyewe, akiwemo 'Aaisha, Talhah na az-Zubayr (R.A) upande mmoja huku dhidi ya 'Ali,'Ammar na maswahaba wengine (R.A). Vita hivyo vikaitwa vita vya al-Jamal (vita vya ngamia), kwa sababu vilipiganwa kwenye sehemu ya ngamia alobeba kiti cha 'Aaisha (R.A).

Vilitokea vita hivyo katikati ya mwezi wa Jumaada al-akhirah, mwaka wa 36H. Ali (R.A) akashinda vita hivyo, lakini baada ya takriban zaidi ya waislamu 10,000 (elfu kumi) wakiwemo Talhah na az-Zubayr waliuwawa. Baada ya kushinda vita hivyo, Ali alimhudumia 'Aaisha kwa heshima na akamshindikiza kwa usalama hadi nyumbani kwake. 'Ammmar Bin Yaasir (R.A.) alisema kwenye khutba aloitoa kabla ya vita hivyo, "Kwa kweli, sisi tunatambua yakwamba, yeye 'Aaisha ni mkewe Mtume wetu (S.A.W) kwenye maisha ya mwanzo na mwisho."

Kuhusika kwa 'Aaisha na wafuasi wake kwenye vita hivyo kumetokamana na ijitihad, na walifanya hayo kwa kumridhisha Mwenyezi Mungu. Lakini, waligundua baadae yakwamba msimamo wao huo ulikuwa ni wa makosa, na akajuta 'Aaisha majuto makubwa mpaka siku zake za mwisho.

MAUTI YA 'AAISHA (R.A.)

'Aaisha (R.A.) aliiwasilisha sehemu kubwa sana ya elimu kutoka kwa Mtume

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

(S.AW.) na idadi ya maswahaba zake, wakiwemo Abu Bakr na Umar (R.A). Masimulizi yake yaliyohifadhiwa ni zaidi ya elfu mbili na mia tatu ambayo yamehifadhiwa katika al-Bukhari, Muslim au wote wawili.

'Aaisha (R.A.) alikuwa ni mwanamke mtoaji, na mkarimu na aliishi maisha ya wastani.

'Aaisha (R.A.) alikufa katika mwaka wa 57H huko al-Madina na akazikwa al-Baaqi'.

ZAYNAB BINT KHUZAYMAH

Bibi Zaynab Bint Khuzaymah Bin Al-Harith Bin 'Abdillah Al-Hilaaliyyah (R.A.) pia akiitwa kwa jina la Umm ul-Masaakin (mama wa maskini) kutokamana na ukarimu wake wa kutoa kwa wingi. Yeye ni nduguye Maimunah kwa upande wa mama.

Awali, aliolewa na at-Tufayl Bin Al-Harith. Baada ya kufa at-Tufayl, aliolewa na nduguye 'Ubaydah Bin Al-Harith. Nae 'Ubaydah aliuwawa kwenye vita vya Uhud, na Mtume (S.A.W), mapema baada ya tukio hilo, akamuowa.

Aliishi na Mtume (S.A.W) kwa takriban muda wa miezi miwili pekee kisha akafariki alipofika umri wa miaka thalathini. Alikuwa ni wa mwanzo miongoni mwa mama za waumini kuzikwa katika makaburi ya al-Baqi'.

UMM-SALAMAH

Nasaba yake
Jina la Umm Salamah (R.A.) lilikuwa Hind Bint Abi 'Umayyah. alitokamana na kizazi cha Makhzum cha kabila la Quraysh. Alikuwa ni binamu wa Khalid Bin Al-Walid na Abu Jahl Bin Hisham. Alikuwa ni mwanamke mzuri sana atokae kwenye nasaba ya kuheshimika mno.
Alikuwa ni miongoni mwa waislamu wa mwanzo wa kike waliohama kuelekea al-Madina kabla ya kuolewa na Mtume (S.A.W), aliolewa na nduguye wa kunyonya, (kulea), Abu Salamah Bin Abd il-Asad Al-Makhzum (R.A).

KUOLEWA KWAKE NA MTUME (S.A.W)

Umm Salamah akahadithia yakwamba siku moja alimsikia Mtume (S.A.W) akisema:**'Pindi msiba unapompata muislamu na akasema kama alivyoamrishwa na Mwenyezi Mungu, "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake yeye tutaregea, Ewe Mwenyezi Mungu, nijazi kwa yaliyonisibu na unipe badala yake kwa yaliyo bora." Basi kwa hakika Mwenyezi Mungu atampa badala yake kwa yaliyo bora.'**

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Hivyo basi, alipokufa Abu Salamah, Umm Salamah akaanza kufikiri, "Ni yupi miongoni mwa waislamu atakuwa bora kuliko Abu Salamah? Yeye alikuwa ni katika wa mwanzo kuhamia kwa ajili ya Mtume (S.A.W)! Mbali na yote hayo aliomba du'a hiyo na Mwenyezi Mungu akamtakabaliya kwa kumpa Mtume (S.A.W) badala ya Abu Salamah. Mtume (S.A.W) alimpa ujumbe Haatib Bin Abi Balta'ah ende akamposee bibi huyu (Umm Salamah) nae akajibu, "Mimi ninae binti yangu (namlea) nami ni mwanamke mwenye wivu (na wewe umeowa wake wengi)." Kwa hivyo Mtume (S.A.W) akasema: **"Amma kuhusu binti yake, tunamuomba Mwenyezi Mungu amtoshelezee kutokamana na yeye (mama). Na namuomba Mwenyezi Mungu amuondoshee wivu alonao."**

Kwenye riwaya nyengine, Umm Salamah (R.A.) ametueleze yakwamba alipokufa Abu Salamah alikwenda kwa Mtume (S.A.W) na akamwambia, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Abu Salamah amekwisha kufa." Mtume (S.A.W) akamwambia aseme: **"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe mimi na yeye na umtangulize yeye badala yangu kwa lilo zuri."** Na akamalizia, "Mwenyezi Mungu kisha akanipa mimi badala yake kwa alo bora kwangu kuliko yeye: Muhammad (S.A.W)!".

Aliolewa na Mtume (S.A.W) katika mwaka wa 4H na hapo alikuwa na umri wa takriban miaka thalathini. Wanawe wote watatu, Umar, Salamah na Zaynab walikuwa maswahaba wa Mtume (S.AW.). Na yeye mwenyewe pia alikuwa ni miongoni mwa wanazuoni wa kiswahaba.

KIFO CHAKE

Umm Salamah alikuwa ni wa mwisho wa mama za waumini kuaga dunia. Aliishi mpaka kufikia wakati wa kuuwawa kwa al-Husayn Bin Ali (R.A). Jambo hilo lilimuhuzinisha sana nae akaaga duniya muda mfupi baada ya tukio hilo. Na hapo ilikuwa ni mwaka wa 61H akiwa na umri wa tisiini kwa makisio. Alizikwa kwenye makaburi ya Al-Baqi`.

HAFSAH BINT 'UMAR

Hafsah (R.A) alikuwa ni binti yake 'Umar Bin Al-Khattaab Bin Nufayl (R.A) kutoka kwenye kizazi cha Quraysh. Mamake alikuwa ni Zaynab Bint Maz'un ambae ni dadake 'Uthmaan Bin Maz'un.

Hafsah aliwahi kuolewa mbeleni na Khumays Bin Hudhaafah as-Sahmi. Huyu Khumays alikuwa ni miongoni mwa waislamu wa mwanzo waliohajiri kwenda al-Habashah (Abyssinia). Alijumuika kwenye vita vya Badr na Uhud, na akafa kutokana na majaraha mapema baada ya vita vya Uhud katika mwaka wa tatu wa al-Hijrah.

Baada ya kifo cha Khumays, 'Umar, akataka kumuoza Hafsah kwa Abu Bakr na 'Uthmaan, lakini wote wakakataa kumuowa. Jambo hilo likamuudhi 'Umar, lakini Mtume (S.A.W) akamtuliza kwa kumwambia:

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

"Mtu alie bora kuliko 'Uthmaan atamuowa Hafsah, na 'Uthmaan atamuowa alie bora kuliko Hafsah." Hafsah alipo-olewa na Mtume (S.A.W) alikuwa na takriban umri wa miaka ishirini. Mtume (S.A.W) alimtaliki(alimwacha) talaka moja, yamkini kwa kufichua siri aloamrishwa kuhifadhi na Mtume (S.A.W) (kama tutakavyoizungumzia hapo chini), lakini Mwenyezi Mungu akamuamrisha Mtume (S.A.W) amrudie. Akasema, **"Jibril ameniambia, "Mrudie Hafsah, kwa sababu anafunga sana na kuswali swala za usiku, nae atakuwa ni mkeo kwenye Jannah (Pepo)."**

Aliaga duniya takriban mwaka wa 41H akiwa Al-Madina.

ZAYNAB BINT JAHSH

Zaynab Bint Jahsh Bin Rayaab (R.A) alikuwa ni binti ya Umaymah bint 'Abd ul-Muttalib Bin Hashim, shangazile Mtume (S.A.W) upande wa baba. Alizaliwa takriban miaka 20 kabla ya kuanza shughuli za Utume.

Alisilimu akiwa Makkah mapema wakati wa harakati za Mtume (S.A.W) na akaozwa Zayd Bin Haarithah, Mawlaa (huria) wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ndoa yao haikufana na ilimalizikia na talaka. Baada ya kuachwa, bila ya kukawiya, ikaja amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu yakwamba Mtume (S.AW.) amuowe. Alikuwa akijivunia kwa hilo na akisema: "Nyinyi muliozwa na wazazi wenu; amma kunihusu mimi, Mwenyezi Mungu Ndie alienioza kutoka juu ya kiti Chake"

Alikuwa ni mke mwema,mwenye huruma na mtoaji. Akasema Mtume (S.A.W): **"Wakwanza miongoni mwenu (wake zangu) atakaejiunga na mimi ni yule mwenye mikono mrefu (mtoaji sana)."** 'Aaisha (R.A) akasema: "Wote wao (Mama za waumini) walikuwa wakishindana katika utoaji, lakini Zaynab alitushinda kwa sababu alikuwa akifanya kazi (akipata pesa) na kisha akizitoa kwa njia ya sadaka." Kwa hivyo, imeelekea yakuwa hadithi hiyo imemhusu yeye, kinyume na baadhi ya waandishi wanavyodhania (kuwa imemuhusu Sawdah).

'Aaisha (R.A.) vile vile akamsifu kwa kusema: "Alikuwa ni mshindani wangu mkubwa katika kujipendekeza kwa Mtume (S.A.W). Sijaonapo mwanamke mwema zaidi ya Zaynab, wala mwenye taqwa ya Mwenyezi Mungu, alo mkweli alo-mkarimu mbele ya jamaa zake, mwenye fadhila, na alo na bidii juu ya kazi aloifanya kwa njia ya sadaqa...isipokuwa kwa hasira alizokuwa nazo, lakini akijizuia kwa haraka. Mwenyezi Mungu amuelee radhi." Hadith hiyo hapo juu yaonyesha yakuwa Zaynab alikufa kabla ya Sawdah. Alikufa mwaka wa 20H na 'Umar(R.A) akamswalia. Alizikwa al-Baqi`.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

JUWAYRIYAH BINT AL-HAARITH

Juwayriyah (R.A) alikuwa ni binti ya al-Haarith Bin Abi Diraar. Alikuwa akiitwa Barrah, lakini Mtume (S.A.W) akalibadilisha jina hilo na kumwita Juwayriyah. Kabila lake ni Al-Mustaliq, na alichukuliwa kama mfungwa wa kivita wakati wa vita vya Al-Muraysi' mnamo mwaka 5H. Alipo-olewa na Mtume (S.A.W) alikuwa na Umri wa miaka ishirini na akafa baada ya takriban miaka 50.

Alikuwa ni mwanamke mrembo sana kama alivyoungama mkewe mwenza 'Aaisha (R.A): "Mtume (S.A.W) alipowagawanya wafungwa wa kivita wa kabila la al-Mustaliq, Juwayriyah Bint al-Haarith alipewa Thaabit Bin Qays Bin Ash-Shammaas (au Binamu yake). Juwayriyah akafanya mkataba nae ili ajikomboe kwa pesa. Alikuwa ni mwanamke mrembo sana, hapana yeyote atakaemuona isipokuwa ataduwaa kwa urembo wake. Alikuja kwa Mtume (S.AW.) kutaka msaada wake ili ajikomboe.

Wallahi, nilipomuona amesimama mlangoni kwangu, nilimchukia (kwa urembo wake), na nikajua tu yakwamba Mtume (S.A.W) ataona kitu kwake yeye nilichokiona mimi (cha urembo). Aliingia ndani akasema,"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi ni Juwayriyah Bint al-Haarith Bin Abi Diraar, kiongozi wa watu wake, na nimeguswa na mkasa kama ujuavyo. Nimegawiwa kwa Thaabit Bin Qays Bin Ash-Shammaas (au Binamu yake). Nimefanya mkataba nae ili nijikomboe, na nimekuja kutaka msaada wako kuhusu jambo hilo. Akasema Mtume (S.A.W), **"Jee, ungelipendelea kupata lilo bora kuliko hilo?"** 'akauliza 'Ni kitu gani hicho, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema Mtume(S.A.W), **"Nitakulipia deni hilo, kisha nikuowe."** Akasema Juwayriyah "Bila shaka! Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Akasema (S.A.W), **"Hilo limeshapita".**

Habari ziliposambaa yakwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu amemuowa Juwayriyah, waislamu wakawaacha huru wale wafungwa wa kabila la al-Mustaliq, ambao wameshakuwa ni shemegi zake. Hivyo basi, jamii mia moja kutoka kwenye kabila la al-Mustaliq ziliachwa huru, na sijawahi kuona mwanamke yeyote aliwahi kuwaletea baraka watu wake zaidi ya Juwayriyah alivyo fanya.

UMM HABIBAH

Jina lake Umm Habibah (R.A) lilikuwa ni Ramlah Bint Abi Sufyaan. Jina la Abu Sufyaan lilikuwa ni Sakhr Bin Harb Bin Umayyah Bin Abd Shams Bin Abd Minaf Bin Qasiyy. Vilevile Umm Habibah alikuwa ni dadake Mu'awiyah Bin Abi Sufyaan.

Alikuwa yeye (Umm Habibah) ni Binamu yake Mtume (S.A.W) kuumeni na alikuwa na uhusiano nae zaidi kuliko wake zake wote. Alihajiri kuelekea al-Habasha (Abyssinia) pamoja na muwewe 'Ubaydullah Bin Jahsh. Walipokuwa al-Habashah, mumewe alirudi na akafa kafiri. Kisha Mtume (S.A.W) akamtumiliza 'Amr Bin Umayyah kwenda kwa an-Najaashi akamuoza Mtume (S.A.W) akampa dirham elfu

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

nne na kumtunukia zawadi na akampeleka al-Madina akiandamana na Sharhabil Bin Hasanah kama mlinzi wake. Aliwasili al-Madina katika mwaka wa sita wa Hijriya, akiwa na umri wa zaidi ya miaka thalathini.

Alikufa chini ya utawala wa nduguye Mu'awiyah mnamo mwaka wa 42 au 44H.

SAFIYYAH BINT HUYAYY

Safiyyah Bint Huyyay Bin Akhtab Bin Sa'yah (R.A) alitokamana na kizazi cha Mtume Harun (A.S.), ambae nae alitoka kwenye kizazi cha Laawi Bin Yaqub Bin Is-haaq (A.S). Hapo awali, Bibi Safiyyah, aliolewa na Salaam Bin Abi al-Haqiq, na kisha akaolewa na ndugu yake Kinaanah Bin Abi al-Haqiq. Kinaanah akauwawa kwenye vita vya Khaybar na Safiyyah akashikwa kama mfungwa wa kivita, lakini Mtume (S.AW) akamuachilia huru na akamuowa. Hapo alikuwa na takriban umri wa miaka kumi n saba.

Alikuwa ni mwanamke bora, mwenye heshima, busara na mke mwema anaependeza. Siku moja, Anas akatuahidithia yakwamba Safiyyah alimsikia Hafsa akimsema kuwa, "Yeya si chochote bali ni binti ya kiyahudi." Akaanza kulia kutokana na matamshi hayo na Mtume (S.A.W) akamuuliza kuhusu kinachomliza. Alipomueleza vile alilyosema Hafsah, Mtume (S.A.W) akasema: **"Kwa hakika wewe ni binti ya Mtume (Harun); na kwa hakika mjombako (Musa) ni Mtume; na kwa hakika wewe mwenyewe umeolewa na Mtume. Kwa hivyo, ni kwa nini anajigamba juu yako?".**

Kisha Mtume (S.A.W) akamwambia Hafsah, **"Mche Mwenyezi Mungu, Ewe Hafsah."**

Alifariki dunia takriban kwenye mwaka wa 50H. akiwa al-Madina na akazikwa al-Baqi`.

MAYMUNAH BINT AL-HARITH

Maymunah Bint Al-Harith Bin Hazn Al-Hilaaliyyah(R.A) alikuwa ni dadake Umm al-Fadhl, mkewe al-'Abbaas. Hivyo basi, alikuwa ni shangazi yake Khalid Bin al-Walid na Ibn Abbaas (R.A).

Kabla ya Uislamu, Maymunah, aliolewa na Mas'ud Bin 'Amr ath-Thaqafi ambae baadae alimuacha. Kisha akaolewa na Abu Ruhm Bin 'Abd il-'Uzza. Alipokufa Abu Ruhm, aliolewa na Mtume (S.A.W) katika mwaka wa 7H, Dhul-Qa'adah mapema baada ya Mtume (S.AW.) kufanya Umrah. Alikuwa ni mwanamke mwenye tabia nzuri sana. 'Aaisha akamsifu kwa kusema: "Wallahi, Maymunah sasa ameshatuondokea. Kwa hakika, hapana shaka yakwamba alikuwa ni muadilifu zaidi miongoni mwetu na mwenye huruma kwa jamaa zake."

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Alifariki mwaka wa 50H na akazikwa Sarif, pambizoni mwa Makkah palepale mahali aliko olewa na Mtume (S.A.W).

MARIYA AL-QIBTI

Mariya Bint Sham'un (R.A) alikuwa ni miongoni mwa watumwa wa kike wa Mtume (S.A.W). Aliekuwa mfalme wa Alexandria na Misri, Al-Muqawqas, ndie aliemtunukia Mtume (S.A.W) Bibi Mariya kama tunu kwenye mwaka wa 7H. Asli yake ni Mqibti kutoka Misri na ana rangi ya kutakata. Alisilimu alipofika al-Madina. Mtume (S.A.W) akamvisha utaji na kumuhifadhi kama wakeze wengine, nae akamzalia kijana akamwita Ibrahim katika mwaka wa 8H. Jambo hili likamfidia kuwa huru. Ibrahim alifariki alipotimia umri wa miaka miwili.

Bibi Mariya alifariki mwaka wa 16H, wakati wa khilafa ya 'Umar (R.A) na akazikwa al-Baqi`

WAKE WENGINE

Kulikuwepo na wanawake wengine walio-olewa na Mtume (S.A.W), lakini kutokana na sababu mbali mbali hakuwahi kuwaingilia. Wanawake hao ni:

1. Al-'Aliyah kutoka katika kabila la Bakr Bin Kilaab.
2. Asmaa' Bint Ka'b al-Jawniyyah.
3. Umm Shariik kutoka kabila la al-Ansaar.
4. Sanaa' Bint Asmaa' Bin as-Salt-as-Sulamiyyah.
5. Fatimah al-Kilaabiyyah.
6. Asmaa' Bint an-Nu'maan al-Kindiyyah.

Amma kuhusu huyo mwanamke wa pili alietajwa hapo juu, 'Aaisha (R.A) akatuhadithia yakwamba al-Jawniyyah alipoingia nyumbani kuonane na Mtume(S.A.W) na Mtume (S.A.W) akamkurubia, alisema,("Audhu Billahi Mink-Najilinda kwa Mwenyezi Mungu na wewe"). Pale pale Mtume (S.A.W) akampa talaka akasema: **"Kwa hakika umeomba ulinzi wa kutoka kwa Alie-tukuka: Nenda kwa jamaa zako".**

Riwaya nyengine ziliashiria yakwamba (Mwanamke huyo) alijuta kwa kitendo hicho maisha yake yote.

TAREHE MUHIMU

Orodha ifuatayo ni muhtasar wa tarehe muhimu kuwahusu Mama zao Waumini. "Ndoa" imekusudiwa mwaka walipo-olewa na Mtume (S.A.W). Ni muhimu kufahamu yakwamba idadi kubwa ya tarehe zilizo andikwa zimekisiwa kuwa karibu na sawa, mpaka watu wa tarekh wakahitilafiana kuhusiana nazo. Kwa mfano, baadhi ya watu wa tarekh wanasema yakwamba Sawdah (R.A) alikufa katika mwaka wa 5H; na

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

wengine wanasema alikufa karibu na mwisho wa khilafa ya 'Umar. Tarehe tulizozipanga hapo chini ni zile zilizodhihiri kuwa sawa kwetu.

Mama Zao Waumini					
#	Jina	Kuzaliwa	Ndoa	Kifo	Umri
1	Khadijah bint Khuwailid	68 KH	28KH	3KH	65
2	Sauda bint Zam'ah	50 KH	2KH	23H	73
3	'Aishah bint Abi-Bakr	08 KH	1KH	57H	65
4	Zainab bint Khuzaymah	26 KH	4KH	4H	30
5	Umm Salamah	29 KH	4KH	61H	90
6	Hafsah bint 'Umar	18 KH	4KH	41H	57
7	Zainub bint Jahsh	33 KH	5KH	20H	53
8	Juwayriyah bint al-Haarith	14 KH	6KH	56H	70
9	Umm Habibah bint Abi Sufyaan	24 KH	6KH	42H	66
10	Safiyya bint Huyayy	10 KH	7KH	50H	60
11	Maymuna bint al-Haarith	30 KH	7KH	50H	80
12	Mariya Bint Sham'un - Mqibti (Mamake Ibrahim)	10 KH	7KH	16H	26

*Maana Ya Herufi "H"- Hijriya; "KH" - Kabla Ya Hijriya